

Sheria gani zimetungwa kuhusu ukeketaji?

By SW - Melkisedeck Shine · April 16, 2022

Ujana na Makuzi | Mapenzi na Ngono Salama

Serikali zote na mashirika ya kimataifa wameweka mdhamana na kukubali kulinda haki za binadamu. Tanzania imetia saini ya mapatano na mikataba ya kimataifa inayohakikisha kuwa kila mtu ana haki kwa afya na haki ya kuwa huru kutokunyanyaswa kwa mfano katika Azimio la Umoja wa Mataifa kuhusu Haki za Binadamu. Maazimio mengine yaliyoboreshwa ili kulinda haki za wanawake na watoto,¹⁵ ni kama lile Azimio la Kuondoa Ubaguzi kwa Wanawake na Azimio la Haki za Mtoto. Maazimio haya yanaeleza wazi kuwa ukeketaji ni desturi mbaya na ni kinyume na haki za binadamu, kinyume cha haki za mtoto na kinyume cha haki za afya kwa wanawake. Na zaidi nchi nyingi za kiasia wamepitisha sheria kupiga marufuku ukeketaji.¹⁶ Hapa Tanzania, Bunge limepitisha sheria maalumu ya Makosa ya Kujamiiiana ya mwaka 1998 ambayo inakataza ukeketaji kwa wasichana na wanawake vijana chini ya miaka 18. Pia kuna sera¹⁷ ambayo inaelezea jamii kuondoa mila na desturi kama vile ukeketaji kwa kuwa zina madhara kwa vijana. Hivyo kama wewe ni msichana chini ya miaka 18 ni kosa la jinai kufanyiwa tohara na pia ni kosa kwa mangariba kujishughulisha na ukeketaji wa wanawake.

Printable AckySHINE Article · <https://ackyshine.com/post.php?post=25662>